



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA



Simu: +255 2602320, 2600891
Nukushi: +2602320, 2602176
Barua pepe: ded@songeadc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Songea,
1barabara ya Halmashauri,
S. L. P 995,
57183 SONGEA, RUVUMA

24/03/2023

TANGAZO

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA ANAPENDA KUVITANGAZIA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU VILIVYO NA SIFA ZA KUPATA MIKOPO ISIYO NA RIBA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023, KUWA WILAYA IMEANZA KUPOKEA MAOMBI YA MIKOPO HIYO ISIYO NA RIBA. KIASI KILICHOTENGWA KWA AJILI YA MIKOPO HIYO NI TZS **154,497,698.31** IKIWA NI 10% YA MAPATO YA NDANI YA WILAYA. HIVYO MNAOMBWA KULETA MAOMBI YA MIKOPO. MAOMBI HAYO YAANZIE NGAZI YA KIJIKI, KATA NA YAHAKIKIWE NA AFISA MAENDELEO YA JAMII NGAZI YA KATA, KISHA YAPITISHWE NA KAMATI YA MAENDELEO YA KATA.

MCHANGANUO WA FEDHA ZILIZOTENGWA KWA VIKUNDI HUSIKA KWA KIPINDI CHA AWAMU YA PILI NI KAMA IFUATAVYO: -

➤ VIKUNDI VYA WANAWAKE	- 61,799,079.32
➤ VIKUNDI VYA VIJANA	- 61,799,079.32
➤ VIKUNDI VYA WATU WENYE ULEMAVU	- 30,899,539.66

VIGEZO

1. KIKUNDI KIWE KIMESAJILIWA KWENYE MFUMO WA UTOAJI WA MIKOPO TPLMIS.
2. KIKUNDI KIWE NA KATIBA INAYOONESHA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA KIKUNDI, KATA, KIJIKI NA KITONGOJI KILIPO KIKUNDI.
3. KIKUNDI KIWE NA MRADI WA PAMOJA NA SEHEMU MAALUM INAYOTAMBULIKA YA KUFANYIA SHUGHULI ZAO (OFISI).
4. UMRI WA VIKUNDI VYA VIJANA NI KUENZIA MIAKA 18-35.

5. KIKUNDI LAZIMA KIWE NA AKAUNTI YA BENKI ILIYO HAI KWA AJILI YA KUPITISHIWA MKOPO.
6. IDADI YA WANACHAMA NA VIKUNDI VYA WANAWAKE NA VIJANA NI KUANZIA WATANO (5) HADI KUMI (10), WALEMAVU NI KUANZIA MMOJA HADI WATANO (5).


VIAMBATANISHO

1. NAKALA YA CHETI CHA USAJILI WA VIKUNDI (CHETI CHA MFUMO WA UTOAJI WA MIKOPO TPLMIS).
2. BENKI STATEMENT INAYOONYESHA AKAUNTI NAMBA YA KIKUNDI.
3. MUHTSARI WA KIKAO CHA KAMATI YA MAENDELEO YA KATA/ KAMATI YA MIKOPO YA KATA.
4. MCHANGANUO WA MATUMIZI WA FEDHA INAYOOMBWEWA MKOPO, TAREHE YA KUANZA BIASHARA/MRADI NA MTAJI WA KIKUNDI WALIONAO.
5. KATIBA YA KIKUNDI.
6. PICHA (PASPORT SIZE) ZA KILA MWANACHAMA.

WOTE WENYE SIFA MNAKARIBISHWA.

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI 07 APRILI, 2023 SAA 9:30 ALASIRI.

IMETOLEWA NA NDUGU



HELLEN SHEMZIGWA

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI

HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA

